



Tulikuwa hatuchukulii maji maji ya kahawia na njano baada ya twahara kuwa ni chochote

Kutoka kwa mama Atwiya radhi za Allah ziwe juu yake, na alikuwa kampa ahadi ya utiifu Mtume rehema na amani ziwe juu yake, amesema: "Tulikuwa hatuchukulii maji maji ya kahawia na njano baada ya twahara kuwa ni chochote".

[Sahih] [Imepokelewa na Abu Daud kwa matamshi haya, na amepokea Bukhari bila ya kuzidisha (baada ya kutwahaika)]

Ameleza swahaba mama Atwiya radhi za Allah ziwe juu yake kuwa wanawake katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake walikuwa hawayazingatii maji maji yanayotoka katika tupu -ambayo yanaelekea katika weusi, au katika njano- baada ya kuona twahara ya kutoka katika hedhi: kuwa ni hedhi, hawaachi swala na swaumu kwa sababu yake.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/10014>

